



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS



TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

MKOA WA KILIMANJARO

Simu : 27-29 74369

Fax : 27- 29 74368

EMAIL :- ded@haidc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Hai,
3BR-TTCL – Kanisani,
25382. Bomang'ombe,
S.L.P. 27,
HAI - KILIMANJARO.
26/09/2023.

TANGAZO LA ZABUNI.

LIMERUDIWA

ZABUNI YA UKUSANYAJI, UZOAJI TAKA PAMOJA NA UKUSANYAJI WA ADA NA
TOZO ZA TAKA KWA MWAKA 2023/2024

ZABUNI NO. LGA/047/2023-2024/HQ/NC/01

1. Halmashauri ya Wilaya ya Hai inatangaza zabuni ya ukusanyaji na uzoaji taka katika maeneo/mitaa yote ya Mji mdogo wa Hai. Zabuni hii ni pamoja na ukusanyaji wa ada na tozo kwa kuzingatia Sheria ndogo ya mazingira ya mwaka 2016 na marekibisho yake ya mwaka 2020.
2. Halmashauri ya Wilaya ya Hai, inapenda kuwaalika watu Binafsi, Ushirika, Makampuni, Taasisi au vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria wenye nia, uwezo na uzoefu wa kufanya kazi hii kutuma maombi yao.
3. Muombaji anapaswa kuwasilisha ombi lake akiambatanisha stakabathi ya malipo ya Tshs. 50,000/= kama ada ya maombi, ambayo haitorudishwa (non-refundable fee).
4. Kitabu cha zabuni (Bidding Document) kinapatikana kwenye Ofisi ya Usimamizi wa Ununuzi Hai siku za kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa. Mwombaji anatakiwa kufika Halmashauri ili apewe "Control Number" ya kulipia.
5. Masharti ya waombaji wa Zabuni.
 - i. Mwombaji awe na Magari maalum ya kubebea taka.
 - ii. Awe na vifaa vya kukusanyia taka
 - iii. Awe na rasilimali watu wa kutosha.
 - iv. Awe na Leseni hai na inayofanana na Biashara husika.
 - v. Usajili wa TIN
 - vi. Uthibitisho wa ulipaji kodi.

- vii. Awe na uzoefu usiopungua mwaka mmoja.
 - viii. Atakayeshinda Zabuni hii atawajibika kuweka Dhamana ya utendaji kazi ya fedha taslimu ya asilimia 15% ya fedha anazotarajia kukusanya kwa miezi ya utekelezaji na malipo haya yatafanyika ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kupokea barua ya kukubaliwa na kabla ya kusaini Mkataba.
 - ix. Mwombaji ataje eneo la Biashara au Kampuni ilipo (Physical location).
 - x. Mwombaji aonyeshe uwezo wa kifedha wa kufanya kazi, aambatanishe Bank Statement ya miezi mitatu ya karibuni
 - xi. Aonyeshe Idadi ya Mashine za POS atakazotumia.
6. Zabuni zijazwe nakala mbili (2), moja iwe halisi na nakala moja zifungwe vizuri katika bahasha ya A4 kwa lakiri na kuandikwa namba ya zabuni, maombi yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wialya ya Hai S.L.P 27 Hai.
 7. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa pamoja na zabuni zitakazotumwa kwenye mtandao (E-mail) hazitapokelewa.
 8. Mwisho wa kutuma maombi ni siku ya Jumatatau tarehe **02/10/2023** saa 04:00 Asubuhi na ufunguzi utafanyika hadharani katika ukumbi wa Halmashauri mara tu baada ya kufunga kupokea zabuni.
 9. Kwa kutokuelewa kipengele chochote unaombwa kufika katika Ofisi ya Usimamizi wa Ununuzi kwa ufafanuzi.

JINSI YA KURUDISHA ZABUNI.

Mwombaji atatakiwa kujaza fomu husika na kutoa maelezo kwa ufasaha kulingana na maelezo yaliyopo katika kabrasha la Zabuni. Kabrasha la Zabuni baada ya kujazwa kama ilivyoelezwa litumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya S.L.P 27 HAI.



DIONIS M. MYINGA
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HAI.

Kny. MKURUGENZI MTENDAJI (W)

HAI